Mkulima Mbunifu

Jarida la Kilimo Endelevu Afrika Mashariki

Toleo la 120 | Septemba 2022

## Yaliyomo

Viatilifu vya asili 2
Umuhimu wa vitamini A 3



Ugonjwa wa minyoo kwa mbuzi 6
MkM imenihamasisha kufanya kilimo hai 7

# Kilimo cha parachichi: Mkombozi kwa mkulima




*Mavuno bora ya parachichi hupatikana kwa uchaguzi bora wa mbegu pamoja na matunzo*

***Kama ilivyo kwa mazao mengine, zao la parachichi ni miongoni mwa mazao yenye gharama nafuu kuzalisha lakini yenye faida lukuki kwa mkulima.***

Kilimo hiki kinaendelea kukua kwa kasi hapa nchini kwani hakihitaji fedha nyingi katika uzalishaji na mavuno huanza kupatikana muda mfupi tu toka kupanda.

Hapa nchini, inaonekana kuwa kilimo hiki kilianza kushika kasi zaidi sana mwaka 2015 na ni mara baada ya kuanza kupatikana kwa mbegu za muda mfupi kama vile hass, fuerte, ndabal ambazo pia zimeonekana kuwa na soko kubwa ndani na nje ya nchi.

Zaidi Uk.4 & 5 »»

## Sikiliza vipindi vya kilimo ikolojia

Kama ilivyo ada *Mkulima Mbunifu* imeendelea kushirikiana na wadau wengine kuhakikisha inakufikishia taarifa sahihi za kilimo hai. Kwa mantiki hiyo, usiache kusikiliza vipindi vya kilimo hai vinavyoletwa kwako na shirika la Farm Radio International kupitia stesheni mbalimbali za radio kama ifuatavyo;

| JINA LA RADIO | JINA LA KIPINDI | NAMBA YA KUBIPU | SIKU YA KIPINDI | | MARUDIO YA KIPINDI | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | SIKU | MUDA | SIKU | MUDA |
| RADIO MWANGAZA | KILIMO NA MWANGAZA | 784105727 | IJUMAA | 2:30-3:00 USIKU | JUMATATU | 2:30-3:00 USIKU |
| RADIO STANDARD FM | KILIMO NA JAMII | 784105733 | JUMAMOSI | 1:00-1:30 JIONI | JUMATANO | 1:30-2:00 USIKU |
| RADIO UTUME | KILIMO NA MKULIMA | 784105788 | ALHAMISI | 2:30-3:00 USIKU | JUMAPILI | 1:00-1:30 JIONI |
| RADIO HABARI NJEMA | JUKWAA LA MKULIMA | 784105711 | JUMAMOSI | 3:00-3:30 USIKU | JUMATANO | 3:00-3:30 USIKU |
| RADIO SAUTI YA INJILI | JICHO LA MKULIMA | 784105718 | JUMAMOSI | 1:30-2:00 USIKU | JUMATANO | 12:00-12:30 JIONI |

## *Mpendwa Mkulima*

*Hakuna mafanikio pasipo jitihada. Ili kufikia lengo fulani kwenye maisha ni lazima kuweka juhudi.*

*Kadri unapowekeza kwenye jambo ulilonuia kufanya katika maisha ni lazima utafanikiwa.*

*Mkulima Mbunifu tumeweza kuweka jitihada katika kuhakikisha wakulima na wafugaji wanapata elimu sahihi ya uzalishaji na kwa wakati ili kuweza kufikia malengo yao ya kiuchumi kwa haraka.*

*Aidha, Mkulima Mbunifu imeweza kushiriki katika maonyesho mbalimbali ikiwemo maonyesho ya wakulima maarufu NaneNane yaliyofanyika katika viwanja vya Themi, Njiro kwa lengo la kuendelea kuweka hamasa na kusikia kutoka kwa wakulima na wafugaji ili kuboresha utoaji wa elimu kulingana na mahitaji ya wanufaika.*

*Tunapenda kuwapongeza wale wote waliweza kushiriki na kutembelea banda letu hasa kwa lengo la kuunga mkono jitihada za utoaji wa elimu kwa njia mbalimbali.*

*Tunatamani kuona wakulima na wafugaji mkitumia fursa mbalimbali mlizoona katika maonyesho hayo kama changamoto kwenu, na kupiga hatua mbele zaidi katika kilimo.*

*Mambo haya yanawezekana pale ukiweka nia na jitihada. Pia kuendelea kuwasiliana na wataalamu husika wa zao unalozalisha.*

*Mkulima Mbunifu tuko kwa ajili yako, kama kuna taarifa zozote unazohitaji toka kwetu basi wasiliana nasi kwa njia za mawasiliano zilizopo katika machapisho yetu nasi tutajitahidi kutafuta ufumbuzi kadri iwezekanavyo.*

Kwa uhitaji wa jarida hili kila mwezi wasiliana nasi kwa kutupigia simu au kwa anwani kwa kupitia barua pepe, facebook, tovuti na sanduku la posta kama zilivyoonyeshwa hapa;

+255 717 266 007
http://www.facebook.com/mkulima_mbunifu
http://twitter.com/mkulima_mbunifu
https://www.instagramu.com/mkulima_mbunifu
mkulimambunifu.org
theorganicfarmer.org
infonet-biovision.org

Wasiliana na *MkM*,
S. L. P 14402, Arusha,
Simu:
0717 266 007, 0762 333 876,
Barua pepe:
info@mkulimambunifu.org
www.mkulimambunifu.org

# Matayarisho ya viatilifu vya asili ya mboga au madini

***Pale ambapo mbinu bora za kilimo zimetumika ipasavyo na bado kuna changamoto za wadudu na magonjwa, hakuna budi viatilifu vya kilimo hai vikatumika au kwa kununua au kutayarishwa na wakulima wenyewe.***

**Method Charles**

Viatilifu ni moja ya pembejeo muhimu ya kilimo, kwani inasaidia katika ukizaji wa mazao haswa pale yanaposhambuliwa na magojwa pia wadudu wasumbufu. Mkulima unaweza kuzuia wadudu kwa kutumia mimea mbalimbali ya asili ambayo inapatikana katika mazingira yanayo kuzunguka. Katika hali ya kawaida sana, wakulima wanaposikia neno kiuatilifu hukimbilia kuwaza kemikali ya viwandani, la hasha1 katika kilimo hai tunazungumzia viuatilifu asili.

Katika picha hapa chini ni orodha ya mimea ambayo inaweza kutumika kama sehemu ya viatilfu asili na wadudu ambao wanaweza kuzuiwa kwa mimea hio.

| Na | Aina ya mimea | Kiasi (Idadi) | Uandaaji |
|---|---|---|---|
| 1 | Majani ya Muarobaini | Kiroba kimoja | Kutwanga |
| 2 | Majani ya Mjenga ua Mlonge | Kiroba kimoja | Kutwanga |
| 3 | Pilipili kali/kichaa | Kilo 1 | Kutwanga |
| 4 | Kitunguu swaumu | Kilo 1 | Kutwanga |
| 5 | Tumbaku asili/ ugoro | Robo kilo au majani 10-15 | Iliyosagwa |
| 6 | Magadi | Kilo 1.5 | Kutwanga |
| 7 | Mnyonyo | Majani 10-15 au mizizi yake | Kutwanga |
| 8 | Karafuu | Kilo 2 | Kutwanga |
| 9 | Mchunga | Majani kiroba kimoja | Kutwanga |
| 10 | Alovera/Mshubiri | Majani 5 - 10 | Kutwanga |
| 11 | Majani ya Mbuyu | Kiroba kimoja | Kutwanga |
| 12 | Utupa | Kiroba kimoja | Kutwanga |
| 13 | Tangawizi | Kilo 2 | Kutwanga |
| 14 | Magamba ya kifuu cha nazi unayatwanga | Kiroba kimoja | Kuchoma na kupata jivu |
| 15 | Pilipili manga | Kilo 1 | Kutwanga |
| 16 | Mapapai machanga | Matatu hadi matano | kukatakata |
| 17 | Sabuni ya unga | Gramu 25 | Kutwanga |
| 18 | Mafuta ya mimea lita 1 | Lita 1 | Changanya baada ya kuchuja dawa yako. |
| 19 | Chumvi ya unga | Nusu kilo | |




Mkulima anaweza kutayarisha dawa ya kukabili wadudu kwa kutumia mchanganyiko wa mimea isiyopungua 18 na hii ni kwa ajili ya kukinga mimea aina zote kwa kufuata njia na taratibu zilizoainishwa hapo juu.

## Matumizi ya dawa hizo

Tafadhali sana usizidishe vipimo isipokuwa kwa mazao ya muda mfrefu kama mananasi, migomba, miti iliyokwisha pandwa kwa muda mrefu shambani. Tafadhali usizidishe kwenye bustani ya maua nyumbani. Dawa hizi zina uwezo wa kuuwa wadudu waharibifu wa mmea na mazao ya aina yoyote na zina uwezo mkubwa pia wa kukinga na kutibu maradhi mengi yasababishwayo na wadudu. Pia zina uwezo wa kutibu, kukinga (ukungu) au kuvu ya majani kwenye mimea yako.

Aidha dawa hizi husaidia zaidi nguvu za ziada kwenye mmea wako ili uweze kukua vizuri.

Mkulima akizingatia kanuni hizi ategemee kwamba atapata mazao mengi na bora, hivyo kuongeza kipato na kuinua hali ya uchumi katika maisha.Karibu viuatilifu vyote vilivyoainishwa hapo juu vinaweza kulimwa na mkulima mwenyewe.

*Mkulima Mbunifu* ni jarida huru kwa jamii ya wakulima Afrika Mashariki. Jarida hili linaeneza habari za kilimo hai na kuruhusu majadiliano katika Nyanja zote za kilimo endelevu. Jarida hili linatayarishwa kila mwezi na *Mkulima Mbunifu*, Arusha, ni mojawapo ya mradi wa mawasiliano ya wakulima unaotekelezwa na Biovision (www.biovision.ch) kwa ushirikiano na Sustainable Agriculture Tanzania (SAT), (www.kilimo.org), Morogoro. Jarida hili linafadhiliwa na Biovision Foundation

**Wachapishaji:** African Insect Science for Food and Health (ICIPE), S.L.P 30772 – 00100 Nairobi, Kenya, Simu: +254 20 863 2000, icipe@icipe.org, www.icipe.org

Mpangilio: Cathbert Msemo 0652 731 123
**Mhariri:** Erica Rugabandana
**Mhariri Msaidizi:** Flora Laanyuni
**Anuani:** *Mkulima Mbunifu*
Sakina, Majengo road, (Elerai Construction Block)
S.L.P 14402, Arusha, Tanzania
Ujumbe mfupi pekee: 0785 496 036, 0766 841 366
Piga simu: 0717 266 007, 0762 333 876
Barua pepe: info@mkulimambunifu.org
www.mkulimambunifu.org



Toleo la 120 | Septemba 2022

# Zingatia umuhimu wa vitamini "A" kwa afya ya mwanadamu

***Vitamini A ni mchanganyiko wa vyakula tofauti pamoja na baadhi ya matunda. Wataalamu wa afya wamekuwa wakisisitiza kila mmoja katika familia ale matunda na mboga za kutosha ilikupata vitamin A ya kutosha katika mlo wake kila siku, ilikuongeza kinga ya mwili, kuongeza uwezo wakufikiri na kupunguza hatari ya magonjwa.***

**Stephano Aminiel**

Ni kwa namna gani Vitamini A inatufanya tuwe na afya iliyobora?

- Inasaidia ukuaji na ufanyaji kazi wa mfumo wa fahamu na ubongo.
- Inasaidia macho kuona vizuri hasa wakati wa usiku.
- Inaukinga mwili wako na magonjwa na kusaidia kupona haraka.
- Inasaidia kuimarisha mifupa, maneno, ngozi na viungo vya ndani kama utumbo na mapafu.

### Vyakula vinavyompatia mwanadamu vitamin A

- **Mboga za kijani iliyokolea kama:** mchicha, matembele, sukumawiki, majani ya maboga na majani ya mlonge.



*Mchicha*

- **Mboga za rangi ya njano na nyekundu kama:** Maboga, viazi vitamu vya rangi ya njano na karoti.



*Viazi vitamu*

- **Matunda ya rangi ya njano na nyekundu kama:** Maembe yaliyoiva, fenesi na mapapai lililoiva.



*Karoti*

- **Mazao ya wanyama:** Mfano nyama nyekundu, maini, figo, samaki na mayai hutupatia vitamin A.



*Nyama*

**Ilikupata Vitamini A ya kutosha katika mlo wako:** inatakiwa kila mmoja katika familia ale matunda na mboga za kutosha kila siku. Hakikisha unachagua mboga zenye rangi mbalimbali (kijani, nyekundu, njano)

- Kwa watoto wachanga chini ya miezi sita hupata vitamin A kutoka kwenye maziwa ya mama.
- Kuchanganya kiasi kidodgo cha nyama au samaki, maboga, au mboga za majani kwenye chakula cha mtoto huongeza kiwango cha vitamin A kwa watoto wenye umri zaidi ya miezi sita.
- Watoto wale mboga na matunda ikiwezekana mara 2-4 kwa siku.
- Vijana na watu wazima wale mboga na matunda ya kutosha kila siku.
- Akina mama wajawazito wanatakiwa kula kiasi kikubwa cha vyakula vyenye vitamin A kila siku.

### Athari za upungufu wa vitamini A

- Kushindwa kuona vizuri hasa kunapokuwa na giza au mwanga hafifu.
- Ngozi kukauka au kupauka na wakati mwingine kuwa na vidonda huku nywele zikikosa afya.
- Kupata maambukizi ya magonjwa mara kwa mara hasa katika mfumo wa njia ya hewa na mfumo wa mkojo.
- Watoto wadogo kuugua surua kwa urahisi.
- Kudumaa kwa watoto kutokana na kukoma kukua na kuongezeka uzito.
- Ukuaji wa taratibu na wenye kasoro wa mifupa na meno.

### Athari za kuzidi kwa matumizi ya vitamini A mwilini

Virutubisho vya vitamini A vikizidi mwilini navyo huweza kupeleka athari mbalimbali kama ifuatavyo;

- Kuhisi kizunguzungu pamoja na kichefuchefu.
- Kuhisi maumivu ya kichwa pamoja na mzio.
- Maumivu ya viungo na mifupaKupoteza fahamu.
- Mtoto aliye tumboni kuumbika kimakosakama mama mjamzito akizidisha matumizi ya dawa zenye vitamini A.
- Kunyonyoka nywele.
- Udhaifu wa mifupa ambapo huweza kupelekea kuvunjiakwa urahisi.
- Kukosa usingizi.



*Maembe*

Toleo la 120 | Septemba 2022

# Parachichi ni tunda lenye faida za kilishe na hukuza kiuchumi

***Parachichi limekuwa tunda mbadala na la kuvutia kwa wakulima wanaopanda miti ya matunda, na kuonyesha uwezo mkubwa kwa wakulima kupata mapato bora.***

**Erica Rugabandana**

Parachichi ni zao linaloonekana kuwa na faida kubwa hasa kipesa na hata kiafya kwani lina vitamin A, C na mafuta kwa wingi. Uhitaji wake umekuwa kwa kasi sana hapa Tanzania. Hii imetokana na kuwepo kwa kampuni za kusafirisha kupeleka nje ya nchi pamoja na kuwepo na viwanda vya kutengeneza mafuta kutokana na parachichi.

## Aina za parachichi

Aina za parachichi zimegawanyika katika makundi mawili ambayo ni kienyeji na kisasa.

Parachichi za kienyeji ni nzuri kulima kwa ajili ya chakula, lakini za kisasa ni nzuri zaidi kulima kwa ajili ya biashara na chakula.

## Aina za parachichi za kisasa

Parachichi ya kisasa ni pamoja na hass, fuerte, ndabal, booth, etinger na waisal.

Aina hizi za parachichi hupendwa sana sokoni kwa kuwa zina kiasi kikubwa cha mafuta au siagi.

**Hass na Fuerte:** Aina hizi za parachichi hukomaa mapema sana. Huchukua miezi sita kukomaa mara baada ya kutoa maua.

Parachichi hizi zina mafuta mengi, lina soko kubwa nan i ndogondogo kiasi cha ukubwa wa gramu 250 hadi 750.

**Ndabal:** Aina hii ya parachichi ina matunda makubwa ukubwa wa gramu 800 hadi kilogramu 1. Huchelewa kukomaa kwani huchukua miezi 8 kukomaa mara baada ya kutoa maua.

**Waisal na Etinger:** Aina hizi za parachichi huvumilia ukame na huchukua miezi 4 hadi 5 kukomaa.

Kuna aina zingine za parachichi ambazo ni;

**Puebla:** Aina hii hutumika na wakulima wengi kwa kuwa ina uimara zaidi na matunda yake hayana nyuzinyuzi na ina uwezo mkubwa wa kukabiliana na magonjwa.

**Singapore:** Hii ni aina mpya ya parichichi ambayo inakuwa kwa haraka sana na kufikia kukomaa katika kipindi cha miezi 15. Inakuwa kwa urefu wa futi 2.

**G5 na G6:** Aina hizi mbili ni maarufu sana kwa kuwa zinafanya vizuri zaidi katika maeneo ya mwinuko na hata katika maeneo ya tambarare. Aina hizi zinaweza kupandikizwa katika aina nyingine zozote za miparachichi ili kuongeza ubora wa matunda.

## Uoteshaji wa mbegu za parachichi

- Mbegu za parachichi za kisasa mara nyingi hushindwa kumudu magonjwa wakati wa uotaji na wakati mwingine huweza kutokuota hivyo inabidi kupandikiza kwenye pandikizi za kienyeji.
- Hatua ya kwanza, unahitajika kukusanya mbegu za kienyeji kutoka kwenye miti mama yaani parachichi zilizoomaa na kuiva.
- Andaa udongo wa kupandia. Udongo huu ni vyema kukusanya kutoka msituni na kuuchanganya na mboji au samadi iliyoiva, majivu, mchanga na maranda au makapi ya mpunga.
- Katika mchanganyiko huo, uwiano wake ni debe 1 la mchanga, udongo debe 2, mboji debe 2, maranda debe 1 na majivu ⅙ ya mchanganyi wote.
- Changanya kwa pamoja huku ukinyunyizia maji kidokidogo kisha jaza kwenye viriba vyenye upana wa inchi 4 na urefu wa inchi 6.
- Otesha mbegu moja moja katika kila kiriba na hakikisha mbegu unayootesha imekauka vizuri na umeondoa maganda.
- Mbegu hii huchukua wiki moja hadi tatu kuota, na mwezi mmoja mpaka kuwa na uwezo wa kubebesha (ili shina la mche liweze kuwa imara). Hakikisha mche umefikia unene wa kalamu ya risasi na urefu wa futi moja.

## Tumia teknologia ya upandikizaji

Upandikizaji hujumuisha aina mbili za mimea. Unachukua mmea mmoja ambao unadhani hauna tija nzuri, na sehemu ya mmea mwingine ambao una ubora zaidi na kupandikiza kwa kukata na kufunga pamoja ili kupata mbegu bora zaidi.

Upandikizaji ni lazima ufanyike wakati mmea umefikisha unene wa penseli. Kupandikiza kwa kutumia chipukizi lililolingana na mche unaopandikizia ni njia yenye mafanikio zaidi.

Upandikizaji ni lazima ufanyike wakati ambao mizizi bado ni laini. Pandikizi litakalotumika wakati wa kupandikiza ni lazima lisiwe katika hatua ya ukuaji kwa wakati huo, na ni lazima umbo liwiane na mti linapopandikizwa. Funga vizuri kwa kutumia nailoni ili kuzuia maji yasipotee na kusababisha pandikizi kukauka.

Mapandikizi ni lazima yatokane na aina ya parachichi ambazo zimeboreshwa kama vile hass, fuerte au pueblo. Kwa wale wakulima ambao wana mkataba na Africado, watahitaji kupata mapandikizi kutoka kwenye miti ya hass. Hii ina maanisha kuwa mkulima anayetaka kuanzisha kitalu kwa ajili ya kupandikiza ni lazima apande walau miti 5 ya parachichi aina ya hass au aina nyingine ya kisasa na yenye ubora ili kupata mapandikizi.



*Mkulima hana budi kuhakikisha anafanya upandikizaji sahihi ili kupata miche bora yenye kupelekea mavuno bora*



*Mkulima Bruno Edward anakuza na kuuza miche ya parachichi kwa wakulima wenzake, katika picha anaonekana akiwa katika shamba lake*

Njia ya kupandikiza ina ufanisi zaidi na ni rahisi kuliko kupanda miche upya, kwa kupandikiza inagharimu chini ya asilimia 75, kuliko kupanda miche upya na kuweza kupata aina ambayo inastahimili magonjwa.

Wakulima pia wamekuwa na rikodi nzuri ya ongezeko la mavuno kutokana na mimea waliyopandikiza, pamoja na upungufu wa matumizi ya madawa.

## Matunzo

Hakikisha unapalilia mara kwa mara ili kuondoa magugu yasiweze kuua miche.

Kama ni wakati wa kiangazi hakikisha unamwagilia maji ya kutosha ili udongo uweze kuwa na unyevu wa kutosha wakati wote.

Upuliziaji wa dawa ni muhimu ili kukinga magnjwa ya ukungu na wadudu kama vile inzi weupe, kimamba wekundu na wengine.

Mara nyingi miparachichi haishambuliwi na wadudu wala magonjwa hivyo upuliziaji unahitajika kufanyika pale panapokuwa na ulazima au kwa kiwango kidogo.

Kila mwaka miti mikubwa na midogo itakapotoa maua, miche nayo itatoa hivyo hakikisha unayaondoa maua hayo.

Mara nyingi mavuno ya miparachi aina za kisasa huanza kukomaa miaka mitatu toka kuanda mche.

## Soko

Soko la parachichi kwasasa limekuwa sana, kutokana na upelekaji wa matunda haya nje ya nchi pamoja na usindikaji wa bidhaa zinazotokana na parachichi.

**Angalizo:** Usioteshe miparachichi kwenye udongo wa mfinyanzi na hakikisha unatumia mbegu zenye ubora.

# Kilimo cha parachichi kimenikomboa kiuchumi

Jina langu ni Bruno Edward, umri wa miaka 38., mkulima kutoka mtaa wa Maheve, mkoa wa Njombe. Mimi ni msomaji wa gazeti la Mkulima Mbunifu ambalo nilipata kutoka kwa jirani yangu ambae anapokea majarida kutoka shirika la CARITAS, jimboni katoliki.

Mimi ni mkulima wa parachichi. Niliona makala ya kilimo cha parachichi katika gazeti, nikavutiwa kusoma kwa umakini zaidi. Nilianza kilimo nikifanya kazi kama msimamizi wa shamba katika shuke ya St. Benedict. Mwaka 2017, nikaamua kuanza upandaji wa miti ya matunda kama maua tu nyumbani katika eneo ndogo. Kati ya hio miche 39 ya kwanza, nilikua na maembe, apple, parachichi na peaches.

## Kwa nini parachichi

Nilisoma kwamba kuna uhitaji wa parachichi. Nikaamua kujikita katika kilimo cha parachichi. Watu walinibeza na kuniambia mambo ni yale yale, kwamba ningelima mazao ya kawaida kama vile pareto na chai, ambayo wakati huo yalikuwa yanayumbayumba. Lakini sikusita kuendelea na kilimo cha parachichi. Nilisoma gazeti na kufanya kilimo hiki kwa lengo la kuuza.

Ninafanya kilimo hiki kwa kutumia mbolea za wanyama na katika tuta ninaotesha mbogamboga ambayo inanisaidia kwa chakula nyumbani, pia kwa vijana wanaonisaidia shambani.

## Mafanikio

Nimeona mafanikio mengi. Nilipoanza, nilikuwa ninauza parachichi debe moja (kilo 20) kwa TShs 5,000 – 6,000. Baada ya miaka 6, nilipata soko la mkataba. Sasa, ninauza kilo 1 kwa TSh 1,500 - 2,000. Kupitia kilimo hcha parachichi, ninasomesha watoto wangu shule na uchumi wangu umeimarika. Pia, ninamiliki nyumba 4 za kukodisha na magari 2; 1 ya mizigo na lingine la kutembelea.

## Ushauri wangu

Ninashauri wakulima wasiwe wanapuuza vitu. Kwa mfano, magazeti kama ya Mkulima Mbunifu yanasaidia sana na huwezi kupata elimu ya bure kama hii. Zaidi, ni muhimu kutokukata tama. Ni vema kuelewa na kufanyia majaribio yaliyomo kwenye jarida ili uweze kufanikiwa.

Nimejifunza kwamba kilimo cha parachichi ni ni mradi wa muda mrefu, ambao unahitaji gharama kubwa za awali wakati wa kupanda, ikifuatiwa na kusubiri kwa miaka 3-5 ili miti ianze kuzalisha. Hivyo, mkulima lazima awe na subira. Ili kupata matunda mazuri, ni muhimu kufanya tathmini kamili kabla ya kuanza na kudumisha shamba lenye afya ambalo hutoa mavuno ya juu kwa miaka mingi.

# Fahamu ugonjwa wa minyoo kwa mbuzi na namna ya kudhibiti kwa dawa za asili

***Afya ya mbuzi hutokana na lishe bora inayopatikana kwa kulisha majani mabichi, majani makavu, vyakula vya ziada vya kutia nguvu, protini, madini, vitamini na maji safi na ya kutosha ya kunywa.***

**Dorothea Chambo**

Usafi wa banda unaojumuisha hori la kulia, vyombo vya kulishia pamoja na ndoo au vyombo vya kunywea maji pia ni sehemu ya kutunza afya ya mbuzi.

Mbuzi anapoachiwa kufanya mazoezi kwa kuzungukazunguka katika banda kubwa lenye nafasi ya kutosha ama kuachiwa huru kwenye uwanja humsaidia kuimarisha afya yake.



*Mbuzi wanatakiwa kutunzwa na kupewa dawa za minyoo mara kwa mara ili kulinda afya yao na kupata mazao bora*

## Minyoo kwa mbuzi

Ugonjwa wa minyoo ni moja ya tatizo kubwa linalowakumba sana mbuzi huku madhara yake yakiwa ni makubwa hasa kupungua kwa kasi ya kukua na hasa kupelekea vifo kwa wale mbuzi wenye umri mdogo.

## Aina za minyoo

- Minyoo mikubwa ya mviringo inayoishi kwenye tumbo na utumbo.
- Minyoo midogo ya mviringo inayoishi pia kwenye tumbo na utumbo.
- Minyoo bapa inayojulikana kama tegu ambayo huishi kwenye utumbo.
- Minyoo inayoishi kwenye maini.
- Minyoo inayoishi kwenye mapafu.

Kati ya jamii hizi za minyoo, aina inayosumbua sana mbuzi ni ile ya jamii za mviringo aina kubwa na ndogo.

## Namna mbuzi wanavyopata minyoo

Kwa kawaida mbuzi huwa na matumbo manne, na utumbo wa nne ambalo ndilo la mwisho na ambako ndiko chakula huanza kufyonzwa na kuingia mwilini ndiko ambako minyoo hupendelea kuishi na kutaga mayai ambayo hutoka nje pamoja na kinyesi.

Mayai hayo yakitoka kupitia kwenye kinyesi, kama hali ya hewa ikiwa nzuri yaani yenye unyevu huanguliwa kisha minyoo midogomidogo hutokea na kuishi kwa kutumia mvuke au unyevu ulioko kwenye nyasi/majani.

Katika nyakati ambazo hazina jua kali minyoo hiyo hujibanza sehemu za juu za nyasi hivyo mbuzi wanapokula nyasi ambazo bado zina umandi basi humeza minyoo hiyo.

Kwa kuwa mbuzi hatafuni nyasi mara tu baada ya kuzikata basi minyoo hiyo huendelea kuwa hai na kuishi katika utumbo wa nne na hatimaye hutaga mayai ambayo baadaye hutoka na kinyesi kisha mzunguko wa maisha huanza tena.

## Dalili zinazoonyesha mbuzi ana minyoo

- Mbuzi huwa na afya mbaya
- Manyoya huwa yamesimama na hayapendezi
- Mbuzi wadogo huharisha
- Hata ikiwa mbuzi amekonda, basi huonekana kuwa na tumbo kubwa
- Mbuzi hupungukiwa damu

## Namna ya kuzuia minyoo

- Mbuzi wapewe dawa yam inga dhidi ya minyoo kila baada ya miezi mitatu na hasa wakati wa masika. Kwa watoto wa mbuzi wenye umri kati ya wiki sita hadi miezi mitano wapewe dawa za kinga ya minyoo kila mwezi.
- Mbuzi wasilishwe kwa kufungwa Kamba mahali pamoja kwa muda mrefu. Kama mfugaji atalazimika kumlisha mbuzi kwa kumfunga kamba, basi abadilishe eneo la kumfunga zaidi ya mara tatu kwa siku na maeneo ya kuchunga yapate nafasi ya kukaa bila mifugo kwa kipindi cha wiki sita.
- Mbuzi wachungwe kwenye maeneo makubwa na siyo sehemu za karibu na nyumba za watu kijijini.
- Mfugaji asisubiri mpaka mbuzi augue ndipo aanze kumshughulikia, hakikisha mbuzi anapewa kinga kumlinda kuugua.

## Dawa za asili za minyoo

- **Lukina/Lusina:** Mbegu za kijani za lukina hutumika kutibu ugonjwa huu, yaani kwa kutwanga mbegu 50 hadi 100 ambazo hazijakomaa kisha kuchanganya na maji na kumpa mbuzi robo kikombe mara mbili kwa siku. Rudia kila baada ya miezi mitatu.
- **Ikumburi (kipare)**: Majani yake hutumika kwa kutwanga na kuchanganya na maji kisha kumpa mbuzi nusu kikombe mara moja kwa siku na kisha kurudia kila baada ya miezi mitatu.



- **Ndulele (Solanum incanum):** Mizizi yake hutumika kwa kutwanga kiasi kidogo kisha kukamua maji yake na kumnywesha mbuzi kama nusu kikombe cha chai.





Toleo la 120 | Septemba 2022

# Ahamasika kufanya kilimo hai baada ya kusoma jarida la MkM

***"Nimejifunza mambo mengi toka jarida la Mkulima Mbunifu hasa kuzalisha kwa misingi ya kilimo hai na nimeweza kutekeleza kwa vitendo ili wengine wajifunze kutoka kwangu".***

**Flora Laanyuni**

Hayo ni maneno ya Bw. Kastuli Paulo toka kijiji cha Tumati, Wilaya ya Mbulu (Arusha), mkulima wa kilimo hai ambaye anajishughulisha na uzalishaji wa mazao mbalimbali kama vile viazi mviringo, mboga za majani ikiwamo chainizi, sukuma wiki, kilimo cha migomba, ufugaji wa ng'ombe, mbuzi na kuku.

Bw. Kastuli anasema kuwa, kupitia jarida la *Mkulima Mbunifu* amehamasika sana kufanya uzalishaji kwa misingi ya kilimo hai hususan kutokana na faida alizojifunza kupitia jarida hili.



*Bw. Kastuli Paulo akionyesha baadhi ya nakala za jarida la Mkulima Mbunifu anazotumia kujifunza juu ya kilimo hai*

## Maisha kabla ya kilimo hai

Bw. Kastuli anasema kuwa, huko nyuma kabla ya kupata jarida la *Mkulima Mbunifu* alikuwa akizalisha kwa kutumia kemikali za viandani ikiwa ni pamoja na sumu kupambana na wadudu, magonjwa pamoja na mbolea za kukuia mimea.

''Nilifanya uzalishaji kwa misingi hii kwa muda mrefu lakini sikuwa nikipata mavuno mengi na ikiwa nitapata mavuno mengi basi gharama niliyotumia lazima ilikuwa kubwa kwani pembejeo za kilimo ziliuzwa kwa bei kubwa lakini ilitakiwa nitumia kiasi kikubwa ili niweze kunufaika''.

## Alianzaje kilimo hai

''Nilianza kupokea majarida ya *Mkulima Mbunifu* mwaka 2020 kupitia MVIWAMA. Niliposoma baadhi ya makala nilihamasika kuanza kufanya uzalishaji kwa misingi ya kilimo hai hasa pale nilipogundua madhara yatokanayo na kemikali za viwandani hivyo nikaanza moja kwa moja kulima mbogamboga na viazi vikuu''alisema.

''Niligundua kuwa kilimo hai si tu kinasaidia kukwepa madhara yatokanayo na kemikali za viwandani lakini inasaidia katika utunzaji wa mazingira, utunzaji rahisi na salama wa mifugo, uzalishaji kwa gharama nafuu, pamoja na upatikanaji wa soko la kuaminika wa mazao wakati wote''aliongeza.

## Anazalisha mazao gani

Bw. Kastulia anasema kuwa anazalisha mazao mbalimbali kama vile mahindi, maharage, kitunguu, viazi mviringo, mbogamboga lakini zaidi anazalisha mbogamboga na viazi mviringo kwa wingi jambo analolifurahia kwani soko lipo na ana uhakika wa chakula salama kwa ajili ya familia yake mwaka mzima.

## Anazalishaje kwa misingi ya kilimo hai

Bw. Kastuli anasema kuwa, kwa kiasi kikubwa anatumia mbegu za asili hasa za mahindi na maharage lakini pia kwa mazao kama vile viazi, mbogamboga ananunua katika maduka ya pembejeo za kilimo yaliyosaliwa na serikali kisha kuyazalisha kwa njia za kilimo hai.

Anasema kuwa, anatumia mbolea za asili hasa baiyoslari inayotokana na kinyesi cha mifugo baada ya kuchakatwa ili kupata moto lakini pia anatumia mboji.

Aidha, anatumia dawa za asili alizojifunza kupitia jarida la *Mkulima Mbunifu* kutibu magonjwa na wadudu waharibufu wa mazao.

## Soko la mazao ya kilimo hai likoje

''Soko la mazao ninayoyazalisha kwa misingi ya kilimo hai linapatikana na mbaya Zaidi nashindwa kumudu wateja kwani huwa wengi kiasi kwamba nakosa cha kuwauzia''.

''Wateja wakubwa ni wanakijiji ambao mara baada ya kuwaelezea kuhusu mazao yaliyozalishwa kwa misingi ya kilimo hai na baada yaw engine kuanza kutumia wamekuwa wakimiminika kila siku kwa ajili ya kununua hasa mbogamboga jambo linalopelekea kutokufikisha mazao sokoni mara kwa mara kwani huisha nyumbani''.

Bw. Kastuli anaongeza kuwa hata akipandisha bei mara nyingi si rahisi kwa wateja kuulizia ni kwanini au kughahiri kununua jambo linalomtia hamasa ya kuzalisha kwa wingi.

## Changamoto

Bw. Kastuli anasema kuwa changamoto kubwa anayoipata ni ukosefu wa mbegu za asili kwa mazao mengine pamoja na wadudu waharibifu wa mazao wa ardhini lakini anashukuru kuwa Mkulima Mbunifu imeweza kujitahidi kwa kiasi kikubwa kuelekeza namna ya kukabilia nao kwa njia rafiki.

## Wito kwa *Mkulima Mbunifu*

''Nawaomba *Mkulima Mbunifu* kuendelea kusambaza majarida haya kwa wingi kwa wakulima wengine pamoja na kutoa elimu juu ya umuhimu wa majarida hayo''.

## Wito kwa wakulima

''Nashauri wakulima wajikite katika uzalishaji kwa njia ya kilimo hai kwani kina faida hasa katika kulinda afya ya mlaji, wanyama, mimea na kudumisha rutuba ya udongo huku ukizalisha kwa gharama nafuu na kupata pato kubwa''.

# Waulizavyo wasomaji wa jarida la MkM kwa njia ya mitandao ya kijamii

***Mara kwa mara tumekuwa tukichapisha maswali na maoni mbalimbali yatolewayo na wasomaji wa jarida hili kwa lengo la kukusidia wewe msomaji kujifunza zaidi kupitia maswali hayo pamoja na kuweza kushirikisha maoni au maswali yako ili kuweza kupata utatuzi.***

**MkM**

Haya ni baadhi tu ya maswali yaliyoulizwa na wasomaji wa jarida hili kwa njia ya tovuti na ukurasa wetu wa facebook.

**Swali toka kwa Christopher Emmanuel:** Naomba kujua dume la bata aina ya pekin likoje

***Jibu toka Mkulima Mbunifu:*** Habari, Karibu *Mkulima Mbunifu* na asante kwa swali lako. Kuhusu namna ya kutambua bata dume aina ya Pekin, 1. Dume hutoa sauti ya chini na ya utulivu tofauti na jike ambaye hutoa sauti kali na kubwa. 2. Mkia wa dume una manyoya ambayo yamejikunja tofauti nay a jike yaliyonyooka.

**Swali toka kwa Desderi Ruta:** Ndugu, sijui nimechelewa kuwajua? Naomba unifahamishe wapi ntapata mbegu sahihi ya nyanya chungu nyeupe. Nilinunua pakiti imechorwa nyanya chungu nyeupe lakini nilipopanda ikatokea tofauti.

***Mkulima Mbunifu:*** Habari, karibu *Mkulima Mbunifu* na asante kwa swali lako na pole kwa changamoto uliyokumbana nayo. Sisi tunajishughulisha na utoaji wa elimu tu kwa njia ya majarida yetu ya kila mwezi na kwa njia hii ya kimtandao yaani ukurasa wa facebook na tovuti. Kuhusu kupata mbegu sahihi ya nyanya chungu, tunakushauri ukanunue kwenye maduka ya pembejeo yaliyopewa kibali na serikali na hakikisha mbegu unayonunua ina uthibitisho wa *TOSCI* yaani Taasisi ya udhibiti ubora wa mbegu, utaona nembo ikionyesha kuwa imeidhinishwa na *TOSCI* na imeandikwa maelezo yote kuhusu mbegu husika.

**Swali toka kwa Bakari Salim:** Naomba kuuliza nguruwe aliye na ugonjwa wa ukurutu unaweza kumuogesha na dawa za kuogeshea ng'ombe.



*Hakikisha unapata nakala yako ya jarida la Mkulima Mbunifu kila mwezi ili kujifunza zaidi kuhusu kilimo hai*

***Jibu toka Mkulima Mbunifu:*** Habari, Karibu *Mkulima Mbunifu* na asante kwa swali lako. Kama nguruwe wako amepata ugonjwa wa ukurutu ni muhimu pia kufahamu ni aina gani ya ukurutu kwani kuna aina mbalimbali za ugonjwa huu. Hii itakusaidia kujua namna ya kupambana kuepuka kupata ugonjwa huu tena mara utakapowatibu. Kuna dawa zinazotumika kwa ajili ya kuogeshea, na dawa hizi ni zile ambazo zina kiini tete kiitwacho Amitraz kama vile *TIXFIX*, *BAMITRAZ* na *TWIGATRAZ*. Pia ugonjwa huu unaweza kutibiwa kwa dawa za sindano yaani dawa aina ya Ivermectin na kwa kuzingatia utaratibu kutoka kwa mtaalamu wa mifugo kwani kila mnyama hupewa dozi tofauti na mwingine.

Ili kukinga nguruwe na ugonjwa huu, hakikisha unafanya usafi wa banda mara kwa mara, kuogesha mifugo kila wakati kulingana na utaratibu unaotolewa na wataalamu wa mifugo, kupulizia banda la mifugo dawa zenye Amitraz ili kuua utitiri.

Ikiwa umegundua kuna mnyama ameanza kuonyesha dalili za ugonjwa huu, mpatie tiba mapema ili kuwakinga wengine na ikiwezekana wapatie na wanyama wengine wote ambao bado hawaonyesha dalili hiyo.

**Swali toka kwa Tumaini Charles:** Habari, nashukuru kwa elemu nzuri ya ufugaji. Swali la msingi ni kwamba, je ufugaji wa kuku kwa kutumia njia ya asili kwa kuwatibu na kuwakinga ni sehemu ya njia bora ya utunzaji wa kuku? na kama sio hivyo ni kwanini?

***Jibu toka Mkulima Mbunifu:*** Habari Tumaini. Karibu sana *Mkulima Mbunifu* na asante kwa kuwa miongoni mwa wadau na wasomaji wa jarida letu la MkM. Ni sahihi kabisa kufanya ufugaji wa kuku kwa nja ya asili ikihusisha kinga/tiba ni njia bora ya ufugaji wa kuku kwani 1. Ni njia salama ambayo haitumii kemikali za viwandani ambazo ni sumu na amabazo baadaye hupelekea madhara kwa mifugo na mlaji 2. Ni njia ya gharama nafuu kwa mfugaji kwani hutumia malighafi zinazopatikana kwenye eneo lake 3. Ni njia mojawapo yenye tija kwa mfugaji kwani uzalishaji wa kuku na gharama za utunzaji ni ndogo hivyo mfugaji atakapouza kuku wake hupata pato kubwa akishatoa matumizi ya utunzaji. 4. Ni njia inayojali uzalishaji kwa misingi ya kilimo hai.


Haki zote zimehifadhiwa ©2022 *Mkulima Mbunifu*